



### Maswali na Majibu

1. Watawala wa Wayahudi walifanya nini kwa kaburi ya Yesu?  
*Walifunika kwa jiwe kubwa na wakaweka walinzi kuilinda.*
2. Nini ilifanyika mapema sana kwa siku ya kwanza ya juma?  
*Kulikuwa na mtetemeko wa nchi na Yesu alifufuka.*
3. Wanawake waliona nini kwa kaburi?  
*Waliona malaika wawili waliowambia kwamba Yesu amefufuka.*
4. Nini ilifanyika kwa Mariamu Magdalene pale kaburini?  
*Aliona mtu na akafikiri ni mtunza bustani. Alimwita, 'Mariamu' hapo akajua kwamba ni Yesu.*
5. Wanafunzi gani 2 walikimbia kaburini? Walipata nini?  
*Petro na Yohana. Nguo walizomzika nazo lakini Yesu hakukuwepo.*
6. Wanafunzi 2 walipata mtu wasiomjua, walimtambuaje kwamba alikuwa Yesu?  
*Walimjua kwamba yeye ni Yesu alipovunja mkate.*
7. Mwanafunzi yupi hakukubali kwamba Yesu amefufuka? *Tomaso.*
8. Yesu aliuliza Petro nini? Alimuuliza mara ngapi? Mbona aliuliza?  
*"Unanipenda?" Mara 3. Alimsamehe hiyo mara 3 aliyomkana.*
9. Nini ndiyo jambo la maana sana kwa historia? *Kufufuka kwa Yesu.*
10. Mbona kufufuka kwa Yesu kuwe na maana?  
*Inapeana njia ya msamaha na wokovu wetu. Sasa Yesu hafi tena na atafufua wafu atakaporudi.*

### Mistari ya kukariri

1 Wakorintho 15:20      Yohana 20:29      Wafilipi 3:10 – 11

### Mazungumzo

Soma 1 wakorintho 15:20 – 23. Zungumza juu ya maana ya hizi mistari na mbona uufuwa Yesu ni wa maana kwa wokovu wetu.

### Kuandika

Andika orodha ya watu waliona Yesu baada ya kufufuka kutoka kwa wafu. Kila mmoja alimtambua Yesu namna gani?


## Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

### Somo la 37 Kufufuka kwake Yesu

**SOMA** Luka 24:1 – 35; Yohana 20; Yohana 21:1 – 18; 1 Wakorintho 15:20 – 23

#### SOMO

Baada ya Yesu kufa, alizikwa haraka haraka kwa kaburi ya Yusufu wa Arimathaya. Ilikuwa jioni. Wanawake waliokuja na Yesu kutoka Galilaya walichungulia ili wajue penye kaburi ilikuwa. Walipanga kurudi baada ya karamu ya Pasaka ili wapake mwili wa Yesu karafuu nyininge.



Mahali Yesu alizikwa ilikuwa kama chumba ndogo yenye ilikatwa kando ya kilima. Ndani kulikuwa na mwamba uliokuwa laini wakuekea mwili. Mlango ulifungwa na jiwe kubwa lililofingirishwa.

Watawala wa Wayahudi walikumbuka kwamba Yesu alikuwa amesema eti atatoka kwa wafu. Walifunika na jiwe kubwa kabisa ili wajue kama mtu alienda ndani ya kaburi na kuiba mwili. Waliweka walinzi kuchunga nje ya kaburi.

Kulipokucha asubuhi mapema, siku ya kwanza ya juma, kulikuwa na mtetemeko wa nchi na malaika alitoa hilo jiwe kwa kufiringisha. Walinzi walitetemeka, wakaanguka chini na kusirahi. Mungu alimfufua Yesu. Walinzi walipoamka walienda kuambia watawala wa Wayahudi. Watawala waliyahonga wale walinzi. Watawala waliambia walinzi waseme uongo kwamba wanafunzi waliiba mwili wa Yesu.



Kulipopambauka, siku hiyo, wanawake walikuja kwa kaburi ili wapake mwili wa Yesu mafuta. Wanawake waliona malaika wawili waliowambia kwamba Yesu amafufuka kutoka kwa wafu. Malaika waliwambia waende kuambia wanafunzi hiyo habari njema. Wanawake walienda haraka sana na kuambia wanafunzi kwamba Yesu amefufuka na kutoka kwa wafu.

Mwanamke mmoja, Mariamu Magdalene hakutoka kwa kaburi. Marimu hakuelewa kilichotendeka. Alifikiria kwamba mtu alikuwa ameiba mwili wa Yesu. Mariamu alibaki kwa bustani akilia. Baadaye aliona mtu. Alifikiria ni mtunza bustani. Alimuuliza kama ameuchukuwa mwili. Yule mtu alisema kwa upole, "Mariamu." Hapo hapo Mariamu alimtambua kwamba ni Yesu. Alikuwa hai tena! Mariamu alifurahi sana.

Wanafunzi hawakuamini walichoambiawa na wanawake. Hawakuamini kwamba malaika aliwambia kwamba Yesu ako hai tena. Petro na Yohana walikimbia wakaenda kwa kaburi. Yohana alifika kwanza. Aliangalia ndani na kuona nguo zenyé Yesu alifungwa zimekunjwa na kuwekwa kando. Baadaye Petro naye aliingia kaburini. Aliona nguo na kitambaa alichofungwa kichwani. Lakini Yesu hakukuwemo kaburini. Hawakuelewa kilichokuwa kimefanyika.

Baadaye siku hiyo, wanafunzi wawili walitembea kwenda kwa kijiji kilichokuwa karibu na Yerusalem. Mtu wasiomjua alijiunga nao kwa hiyo safari. Yule mtu aliwaaliza sababu gani walikuwa na huzuni. Wanafunzi walimwambia juu ya Yesu na alisulibiwa. Wanafunzi walimwelezea kwamba wanawake walikuwa wamepata kaburi wazi na kwamba Yesu mwenyewe amefufuka kutoka kwa wafu. Mtu yule aliwaelezea kwamba ilibidi Yesu ateswe, afe, afufuke tena na atoke kaburini. Mtu yule aliwaelezea unabii wa Agano la Kale uliozungumza habari yenye imefanyika.

Walifika kwa kile kijiji giza ikiingia. Wanafunzi walimkaribisha mtu yule akae nao. Walikaa mezani wote kula chakula. Yule mtu alichukua chakula akakimega, akashukuru na kuwapa. Papo hapo wakamtambua. Ni Yesu! Yu hai tena! Yesu alitoweka. Wanafunzi walikimbia kurudi Yerusalem ili waambie wanafunzi wenzao habari njema.

Wanafunzi walikutana usiku huo. Walikutana kwa urofa. Walifunga mlanga kwa sababu waliogopa watawala wa Wayahudi. Bunde tu Yesu alisimama katikati yao. Yesu yu hai! Sasa waliamini kwamba Yesu kweli yu hai tena.

Lakini Tomaso mmoja wa wanafunzi hakuwepo. Tomaso hakuona Yesu. Wanafunzi wenzake walimwambia kwamba wamemwona Yesu. Tomaso hakuamini. Baada ya juma moja, Yesu aliwakujia tena. Wakati huu Tomaso alikuweko. Yesu alimwambia, "Angalia! Weka kidole chako kwa alama za mikono yangu. Weka mkono kwa alama ya ubavu. Usiwe mtu asiyeamini."

Yesu aliambia wanafunzi warudi Galilaya. Siku moja wanafunzi wakaenda kuvua samaki. Usiku mzima hawakupata chochote. Asubahi ilipofika, mtu aliwaita kutoka ukingo wa bahari. "Tupa wavu yenu upande wa kulia wa mashua." Papo hapo wavu ilijaa samaki. Ni Yesu ako kando ya bahari! Yesu aliwatangenezea kiamsha kinywa. Yesu aliuliza Petro maraa tatu, "Unanipenda?" Kila alipouliza Petro alijibu kwamba anampenda. Petro alikuwa amemkana mara tatu. Ilimaanisha Yesu alikuwa amemsamehe.

Wanafunzi walikaa Galilaya majuma sita. Walipokuwa kule, walimwona Yesu mara nyangi sana. Yesu aliwafunza mambo mengi kutoka kwa Biblia. Aliwaeleza mambo mengi yenye hawakuwa wanajua hapo awali.

### **UMUHIMU WA UFUFUO**

*Kufufuka kwa Yesu kulikuwa ni jambo la maana katika historia. Kufa na kufufuka kwa Yesu kulitimiza ahadi za Mungu.*

*Katika maisha ya Yesu yote alishindana na majaribu. Yesu alishinda dhambi zote. Aliishi maisha matakatifu isiyo na mawaa. Alipeana maisha yake kama dhabihu iliyotakatifu katika kifo chake msalabani. Yesu alitupea sisi njia ya msamaha wa dhambi*

*Yesu alifufuliwa kutoka kwa wafu. Hatakuwa tena. Yesu anaishi milele. Yesu atakaporudi hapa duniani, atafufua wote walioamini kwa Mungu. Atapeana maisha ya milele kwa wote waliokuwa na imani kwa Ufalme wa Mungu.*